

Uamilifu wa Mofu {-i-} katika Kiswahili Kinachozungumzwa nchini Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo

Dieudonné Butoyi¹ na Anitha Nduwamahoro²

DOI: <https://doi.org/10.56279/mulika.na44t2.4>

Ikisiri

Makala hii inachunguza uamilifu wa mofu {-i-} katika Kiswahili kinachozungumzwa nchini Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Data zilizotumiwa zilikusanywa kutoka katika vipindi mbalimbali vya lugha ya Kiswahili vya redio zinazosikika mjini Bujumbura nchini Burundi, na Uvira, Bukavu na Goma katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Redio husika ni Redio-Televisheni ya Taifa ya Burundi (Radio-Télévision Nationale du Burundi, RTNB), Redio-Televisheni Isanganiro (Radio Télévision Isanganiro), Redio Bonesha FM, Redio Maendeleo ya Bukavu Kusini na Redio ya Umma ya Kivu Kusini (Radio Communautaire Thématique). Mbinu ya usikilizaji makini katika kusikiliza redio na uandishi zilitumiwa katika kukusanya data ambazo zilichanganuliwa kwa njia ya uchambuzi wa maumbo ya maneno. Nadharia ya Mofolojia ya Muunganiko wa Mofu ya Fradin (2003) na Nadharia ya Umiliki na Ufungati ya Chomsky (1981) ndizo zilizoongoza utafiti huu. Uchunguzi wa data ulidhihirisha mambo kadhaa. Kwanza, mofu {-i-} ambayo kwa kawaida wingi wake ni {zi-} huweza kuwakilisha ngeli zingine zozote katika neno husika na kuwa kibadala chake. Pili, matumizi ya mofu {-i-} hayazingatii idadi, hali ambayo huifanya kuashiria ama umoja au wingi. Tatu, huwa na uamilifu wa kiambishi cha upatanisho wa kisarufi. Kutokana na matokeo ya utafiti huu, ingawa mofu {-i-} ina uamilifu wa kimofosintaksia, hudhihirisha kutopatana kwa vipashio vya tungo katika Kiswahili kinachozungumzwa nchini Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

1.0 Utangulizi

Lugha ya Kiswahili, kama zilivyo lugha nyingi za Kibantu, ni ambishi ambayo maneno yake hujengwa kwa mizizi inayofungamana na viambishi vingine vinavyotofautiana kiuamilifu, lakini vinavyoshirikiana ili kulipa neno uarifishaji mkamilifu (Matinde, 2018; Mutaka, 2000). Hivyo, katika Kiswahili, neno ambalo kwa kawaida ndilo kitovu cha uchunguzi wa kimofolojia, huundwa kwa viambishi ambavyo wakati mwingine baadhi yake hudhihirisha upatanisho wa kisarufi baina ya maneno yanapofuatana kuunda sentensi. Katika lugha ya Kiswahili, kama ilivyo katika lugha nyingine za Kibantu, vipashio vinavyosimamia upatanisho wa

¹ Mhadhiri Msaidizi, Idara ya Lugha na Tamaduni za Kiafrika, Kitivo cha Sayansi za Jamii, Chuo Kikuu cha Burundi, Burundi, Barua pepe: dbutoyi17@gmail.com

² Mhadhiri Msaidizi, Idara ya Kirundi-Kiswahili, Taasisi ya Ualimu, Chuo Kikuu cha Burundi, Burundi, Barua pepe: nduwanith@gmail.com

kisarufi ni viambishi ngeli vinavyotokana na ngeli ya nomino iliyopo katika sentensi ambayo vipashio vingine vinatokana nayo (Habwe na Karanja, 2012). Hivyo, upatanisho wa kisarufi hudhahirishwa na viambishi ngeli vinavyoathiri maneno yanayoandamana na nomino husika. Hii ina maana kuwa, ngeli huwa na uamilifu wa kimofosintaksia kwani nomino hutawala upatanisho wa kisarufi kiasi kwamba maneno yanayounda sentensi na ambayo yana uhusiano na nomino huchukua viambishi ngeli kulingana na ngeli ya nomino hiyo.

Katika muktadha wa tofauti mbalimbali za kiisimu zinazotabirika ndani ya lugha fulani, hasa kutokana na umbali wa kijiografia unaowatenganisha wazungumzaji wa lugha hiyo, tofauti za kimofolojia huwa miongoni mwa sifa za msingi zinazobainisha lahaja au launi za lugha hiyo (Bakari, 2015). Hivyo, tukizingatia Kiswahili kinachozungumzwa nchini Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na ambacho kinalengwa na utafiti huu, miongoni mwa sifa za kiisimu zinazokitambulisha, kuna sifa za kimaumbo (Nshimirimana na wenzake, 2020). Kwa mfano, watafiti hao walitambua matumizi ya kipekee ya mofu {-ag-}, hali ambavyo imebainika kama sifa maalumu ya kimofolojia katika Kiswahili hicho. Pamoja na matumizi ya mofu hiyo yaliyogusa mioyo ya watafiti hao, wazungumzaji wa Kiswahili wa Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo hudhahirisha matumizi ya mofu {(-)i-}. Mofu hiyo inajitokeza katika tungo au sentensi za Kiswahili cha Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Hata hivyo, hakuna utafiti wowote uliobainisha dhima za mofu hiyo, jambo ambalo liliamsha ari kwa waandishi ya kushughulikia dhima zake. Waandishi wa makala hii wamejiuliza juu ya uamilifu wa mofu hiyo ambayo haidhahirishi utofauti wa kimatamshi ikizingatiwa ujitokezaji wake katika muktadha wa kimofosintaksia.

Hivyo, makala hii inachunguza uamilifu wa mofu {(-)i-} ambayo inajidhahirisha katika Kiswahili hicho kinachozungumzwa nchini Burundi na Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo. Nchi hizo zinapakana na, kijiografia, ziko Afrika ya Kati ambako lugha ya Kiswahili inatumiwa. Matumizi tofauti ya mofu hii katika Kiswahili cha maeneo hayo yamewahamasisha waandishi wa makala hii kuchunguza uamilifu wake, hasa kimofosintaksia, na nafasi inapojitokeza katika sentensi za Kiswahili cha maeneo hayo.

2.0 Tafiti Tangulizi

Tafiti mbalimbali zilishafanyika zikishughulikia uamilifu wa mofu katika lugha. Nshimirimana na wenzake (2019) walishughulikia uamilifu wa mofu {-ag-} ya Kingwana. Ukusanyaji wa data ulihusisha sentensi mia mbili (200) ambazo zilipatikana kutoka kwa wazungumzaji wa Kiswahili wa mjini Bujumbura. Matokeo ya uchunguzi yalibainisha mambo matatu. Kwanza, {-ag-} ni mofu tamati ambayo inaweza kujiunga na kiishio {-a} na kupata muundo wa {-ag(a)} katika baadhi ya vitenzi. Pili, {-ag-} ni mofu tamati ambayo hudhahirisha hali ya kutokamilika kwa tendo ambapo ndani yake kunadhahirika mara moja hali ya

kuendelea na kutokamilika kwa tendo na hali ya mazoea. Tatu, mofu {-ag-} inajidhihirisha kama kinyume cha mofu {-meisha-} ambayo inadhihirisha hali timilifu katika Kingwana.

Naye Mwashota (2017) alijadili uamilifu wa mofu njeo na athari zake katika fonolojia ya lugha ya Shimalila (M20). Kwa upande mmoja, matokeo ya utafiti huu yalibainisha ujitokezaji wa pekee wa mofu njeo za wakati tofauti na lugha ya Kiswahili. Hivyo, katika Shimalila, viambishi vya njeo hujitokeza ama kabla au baada ya mzizi, jambo ambalo halipo katika Kiswahili. Kwa upande mwingine, utafiti huu ulionesha kuwa, wakati mwingine, upachikaji wa viambishi njeo vya lugha ya Shimalila huhusisha taaluma za mofolojia na fonolojia.

Hassan (2016) alichunguza ujidhihirishaji wa mofu za nafsi na njeo katika Kiswahili akilinganisha Kiswahili sanifu na lahaja ya Kipemba. Alilenga pia kuchunguza namna mabadiliko ya kimofonolojia yanavyoathiri maumbo ya mofu nafsi na njeo baina ya Kiswahili sanifu na lahaja ya Kipemba. Matokeo ya utafiti huu yalionesha tofauti kubwa ya udhihirikaji wa mofu nafsi na njeo kati ya Kiswahili sanifu na Kipemba, kwa sababu idadi ya mofu za Kipemba huwa ni kubwa kuliko idadi ya mofu za Kiswahili sanifu. Kulidhihirika pia tofauti ya mwonekano wa maumbo ya mofu nafsi na njeo, namna zinavyotenda kazi katika kitenzi na mabadiliko ya kimofonolojia yanayoathiri muundo wa msingi wa mofu nafsi na njeo katika Kipemba.

Vilevile, Ally (2020) alichunguza na kuchanganua kuathiriana kwa mofu ambishi na nyambulishi katika uundaji wa vitenzi vya Kisambaa ambapo palidhihirika mashartizuizi yanayotawala uambikaji wa mofu katika kitenzi cha Kisambaa. Matokeo ya utafiti huo yalionesha kuwa mofu ambishi na mofu nyambulishi katika kitenzi cha Kisambaa huathiriana zinapoambikwa katika mzizi wa kitenzi hicho. Mofu ambishi na nyambulishi zinazoathiriana ni pamoja na mofu ya mofimu ya njeo, ukanushi, masharti, kutendea, utendeshi, ufanyikaji sana, kutendeka na mofu ya mofimu ya urejeshi.

Tafiti tanguzizi tulizozipitia hapo juu zinadhihirisha uamilifu wa mofu za aina mbalimbali katika lugha tofauti za Kibantu, kikiwamo Kiswahili. Tafiti hizo zilijikita hasa katika kueleza uamilifu wa mofu hizo, kulinganisha mofu za lugha fulani na lahaja zake kama Kiswahili na lahaja ya Kipemba. Pia, tafiti hizo zilibainisha mazingira ya utokeaji wa mofu katika neno na athari zinazotokana na mazingira ya kifonetiki. Hivyo, mazingira ya utokeaji wa mofu katika kitenzi au neno fulani yanaendana na uamilifu wa mofu husika. Imedhihirika pia kuwa mazingira ya utokeaji wa mofu hutawala mabadiliko ya maumbo ya mofu kutokana na kuathirika na maumbo yanayoandamana nayo.

Licha ya kufanyika kwa tafiti hizo, kwa upeo wa wandishi wa makala hii, hakuna utafiti ulioshughulikia mofu zinazowakilisha ngeli za nomino ukilenga hasa ngeli fulani ya nomino na matumizi yake ya kipekee. Pia, hakuna andiko lililozungumzia mofu {-i-} kwa namna moja au nyingine. Hivyo, makala hii imejikita katika kuchunguza uamilifu wa mofu {-i-} katika Kiswahili kinachozungumzwa nchini Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, ambayo kwa kawaida huwa na umbo {-zi-} kama wingi wake.

3.0 Nadharia ya Utafiti

Utafiti uliozaa makala hii uliongozwa na nadharia mbili ambazo ni Nadharia ya Mofolojia ya Muunganiko wa Mofu kama inavyoelezwa na Fradin (2003) na Nadharia ya Umiliki na Ufungati ya Chomsky (1981). Kwa mujibu wa Nadharia ya Mofolojia ya Muunganiko wa Mofu, ishara ya kileksika ni muunganiko wa kiulalo wa vipashio vidogo kabisa ambavyo vinaitwa mofu. Mofu hizo hulazimika kuungana kiuthabiti kwa namna ambavyo hufuata sheria za muundo wa nje wa neno zinazoongoza matamshi. Ili mofu yoyote inayoshiriki katika muundo wa neno ihakikishwe hivyo, ni lazima itimize masharti mawili. Kwanza, mofu yoyote itambulike kama kipande kidogo kabisa kinachopatikana katika lugha husika na chenye muundo unaotimiza masharti ya uunganishaji wa fonimu katika lugha hiyo. Pili, kipashio hicho kibebe mofimu isiyo/zisizobadilikabadilika kikiwa katika mazingira yaleyale ya utokeaji. Nadharia hii imetumiwa katika kuchunguza maumbo ya maneno ili kuonesha mazingira ya utokeaji wa mofu {-i-} miongoni mwa maumbo mengine na namna yanavyochochea uamilifu wake.

Nadharia ya Umiliki na Ufungati ina mihimili miwili. Mhimili wa kwanza unazingatia sifa za sarufi bia na wa pili ni wa upatanifu. Mhimili wa kwanza huchukulia kuwa kanuni zilezile za kisintaksia hutumika katika lugha zote ingawa sheria hizo zinaweza kutofautiana kidogo kutokana na lugha husika. Mhimili wa pili unafafanua uhusiano wa kimuundo kwa kubainisha sheria ambazo huunganisha vipashio vya sehemu ya sentensi na miktadha ambamo uhusiano huo wa kiunganifu hutumika. Nadharia zote mbili zimetumika pamoja ili kukamilishana. Hivyo, Nadharia ya Umiliki na Ufungati imeshirikiana na ile ya kwanza kwa kuzingatia hasa mhimili wa pili ili kuchunguza namna maneno kama vile nomino na vitenzi, na nomino na vivumishi vilivyoungana, na jinsi mofu {-i-} ilivyosimamia upatanisho wa kisarufi.

Kama ilivyogusiwa hapo juu, sababu ya matumizi ya nadharia hizo mbili ni pamoja na kukamilishana kwa nadharia hizo kwa kuwa Nadharia ya Mofolojia ya Muunganiko wa Mofu imehusika katika uchambuzi wa kimofolojia, ilhali Nadharia ya Umiliki na Ufungati imehusika katika kuchunguza muunganiko wa vipashio.

4.0 Mbinu za Utafiti

Data za utafiti uliozaa makala hii zilipatikana kutoka katika vipindi na taarifa za habari zinazopitia kwenye vituo mbalimbali vya redio vya nchini Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ambazo zinasikika mjini Bujumbura. Redio na vipindi husika vilichaguliwa kwa usampulishaji usio nasibu. Redio hizo ni pamoja na Redio-Televisheni ya Taifa ya Burundi (*Radio-Télévision Nationale du Burundi, RTNB*), Redio-Televisheni Isanganiro (*Radio Télévision Isanganiro*), Redio Bonesha FM kutoka Burundi. Zinazosikika kutoka nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ni Redio Maendeleo ya Bukavu Kusini na Redio ya Umma ya Kivu Kusini (*Radio Communautaire Thématique*). Kwa ujumla, taarifa za habari na vipindi vilivyorekodiwa ni 10 vikiwamo: “Kipindi cha Salamu”, “Kipindi cha Jambo na Majambo” na “Kipindi cha Biashara na Wafanyabiashara”. Mbinu za usikilizaji makini na uandishi zilitumiwa katika kukusanya data. Sentensi mia moja (100) zenye matumizi ya mofu {-i-} ndizo zilizofanyiwa uchunguzi. Watafiti walizichanganua data na kuziwasilisha kwa kutumia mkabala wa kimaalezo na, hivyo, kubainisha uamilifu wa mofu {-i-}, yaani kazi za mofu {-i-} katika sentensi teule.

5.0 Matokeo ya Utafiti

Sehemu hii inawasilisha uchambuzi wa baadhi ya sentensi miongoni mwa sentensi 100 zilizokusanywa. Pia, katika sehemu hii kumjadiliwa mambo mbalimbali ambayo kwa ujumla yanaonesha uamilifu wa mofu {-i-}. Katika kuwasilisha data, kila sentensi husika imefuatiwa na, kwanza, uchanganuzi wa mofu zinazounda neno linalohusishwa na uchambuzi wa mofu {-i-} na, pili, tafsiri yake katika Kiswahili sanifu.

5.1 Utambuzi na Mazingira ya Utokeaji wa Mofu {-i-}

Miongoni mwa sentensi mia moja (100) ambazo zinaunda sampuli ya data ya utafiti huu, sentensi mbalimbali zimedhihirisha mofu {-i-} ikijitokeza mwanzoni mwa kitenzi kama kiambishi ngeli. Katika muktadha huu wa kisarufi, mofu {-i-} inajenga wingi wake katika mofu {-zi-} hasa katika Kiswahili sanifu. Data Na. 1 na 2 zinaonesha jinsi mofu hiyo ilivyojitokeza katika nafasi hiyo.

Data Na. 1

(a) Mradi *inaongelea* nini?

Mofu undaji: {i-na-onge-le-a}

→ Mradi (huo) unahusu nini?

(b) Formation *inamsaidia* kujikomporte mzuri.

Mofu undaji: {i-na-m-saidi-a}

→ Elimu inamsaidia kujiheshimisha.

(c) Mnaweza kufanya nini wakati kanisa *inajaa*?

Mofu undaji: {i-na-ja-a}

→ Mnaweza kufanya nini kanisa linapojaa?

Data Na. 2

(a) Mwisho wa matango ambazo *zilikuletewa* na mimi.

Mofu undaji: {zi-li-ku-let-ew-a}

→ (Huu ndio) mwisho wa matango ambayo yaliletwa kwenu nami.

(b) Jina zake *ziliandikwa* kwa sababu ya nyimbo zake.

Mofu undaji: {zi-li-andik-w-a}

→ Jina lake liliandikwa (lilijulikana) kwa sababu ya nyimbo zake.

Katika Data Na. 1(a-c), mofu {(-)i-} imejitokeza mwanzoni mwa kitenzi kama kiambishi ngeli kipatanishi baina ya nomino-kiima na kitenzi. Kwa kawaida, katika lugha ya Kiswahili, mofu hii inawakilisha nomino ambazo huanza na fonimu /n/ katika umoja na wingi, au nomino mkopo ambazo zinabaki hivyo katika umoja na wingi. Kutokana na mifano hiyo ya Data Na. 1 na 2, mambo mawili yametambulika. Kwanza, ni dhahiri kuwa nomino ambazo zimeshirikishwa na mofu {(-)i-} ni zile ambazo, kwa kawaida, si za ngeli ya {I-ZI}. Hivyo, katika Data Na. 1(a), nomino husika ni *mradi* ambayo ni ya ngeli ya {U-I}, ilhali katika Data Na. 1(c), nomino husika ni *kanisa* ambayo ni ya ngeli ya {LI-YA}. Pili, mofu {(-)i-} imeshirikishwa na kitenzi *inamsaidia* {i-na-m-saidi-a} ikitokana na nomino *formation* iliyokopwa kutoka lugha ya Kifaransa.

Kwa upande mwingine, katika Data Na. 2(a) na 2(b) kulijitokeza wingi ambapo mofu {(-)i-} imejenga wingi katika {(-)zi-}. Jambo ambalo limeshirikishwa ni kwamba, mofu {(-)zi-} imeshirikisha nomino *matango* katika Data Na. 2(a), na *jina* katika Data Na. 2(b) ambazo si za ngeli ya {I-ZI} kwani, nomino *matango* na *jina* ni za ngeli ya {LI-YA}. Data zifuatazo zinaonesha mofu {(-)i-} ikiwa katika nafasi ya kiambishi awali mtendwa.

Data Na. 3

(a) Ile sujet *tutaigabura* namna gani?

Mofu undaji: {tu-ta-i-gab-ur-a}

→ Lile jambo tutaligawaje?

(b) Franga *tutaigabura* namna gani?

Mofu undaji: {tu-ta-i-gab-ur-a}

→ (Hizi) pesa tutazigawaje?

Katika Data Na. 3(a-b), mifano hiyo imeonesha kuwa Waswahili wa maeneo husika hudhahirisha ujitokezaji wa mofu {(-)i-} katika muundo wa kitenzi, kama ilivyo kawaida ya kitenzi cha Kiswahili. Hivyo, katika kitenzi *tutaigabura* {tu-ta-i-gab-ur-a} kwenye Data Na. 3(a) na 3(b), mofu {(-)i-} imejitokeza baina ya mofu njeo ya wakati ujao {-ta-} na mzizi wa kitenzi {-gab-} ikiwa kiambishi mtendwa. Kwanza, katika Data Na. 3(a) mofu {(-)i-} imejitokeza ikiwakilisha nomino *sujet* ambayo mzungumzaji ameikopa kutoka Kifaransa. Pili, katika Data Na. 3(b), mofu {(-)i-} imehusika ikiwakilisha nomino *franga* ambayo nayo ni nomino ya

Kiswahili ila iliyokopwa kutoka lugha ya Kifaransa. Data zifuatazo zinaonesha namna mofu {(-)i-} inavyohusika kama kipatanishi cha ngeli baina ya nomino na kivumishi.

Data Na. 4

- (a) Atayimba nyimbo *yake* ya kwanza.
Mofu undaji: {*i-ake*}
→ Ataimba wimbo wake wa kwanza.
(b) Bajirani *yangu yote* mlale bien.
Mofu undaji: {*i-angu*}/{*i-ote*}
→ Majirani zangu nyote, laleni salama.

Data Na. 5

- (a) Recomandation ndo ninakuwa nayo kwa *hii* mafundisho...
Mofu undaji: {*hi-i*}
→ Hili ndilo pendekezo nilililokuwa nalo kwa haya mafundisho...
(b) Wasikubali kufanya (*h*)*iy*o kazi...
Mofu undaji: {*hi-i-o*}
→ Wasikubali kufanya hiyo kazi...

Data Na. 6

- (a) Madivision ya commerce na *ingine* madivision...
Mofu undaji: {(i)-ingine}
→ Sekta mbalimbali za ufanyaji biashara, na sekta zingine ...
(b) Kupima projet *yote* itapita.
Mofu undaji: {*i-ote*}
→ Kuchunguza mradi wote utakaopatikana.

Data Na. 7

- (a) Tumerepondre tu question ya (*h*)*uyu*.
Mofu undaji: {*i-a/huyu*}
→ Tumejibu swali la huyu tu.
(b) Ataimba nyimbo *yake* ya *kwanza*.
Mofu undaji: {*i-a/kwanza*}
→ Ataimba wimbo wake wa kwanza.
(c) Inakuwa article ya *wapi*?
Mofu undaji: {*i-a/wapi*}
→ Hilo ni andiko la wapi?

Katika Data Na. 4(a) na 4(b), mofu {(-)i-} imejitokeza katika vivumishi vinavyoandamana na nomino na imejitokeza mwanzoni mwa kivumishi kimilikishi *yake* {*i-ake*} ambacho kimeshirikiana na nomino *nyimbo* ambayo iko katika wingi, umoja wake ukiwa ni *wimbo*. Vilevile, katika Data Na. 4(b), mofu {(-)i-} imejitokeza mwanzoni mwa kivumishi kimilikishi *yangu* {*i-angu*} na kivumishi cha pekee *yote* {*i-ote*}; vivumishi vyote viwili vikishirikiana na nomino *bajirani*. Katika Data Na. 5(a) na 5(b), mofu {(-)i-} imejitokeza katika vivumishi

vioneshi *hii* {hi-i} na *hiyo* {hi-i-o} ambapo kutokana na ukaribu au umbali, imejitokeza mwishoni kabisa katika kudhihirisha nafasi ya karibu na kabla ya shina oneshi {-o} katika kuonesha nafasi ya mbali kidogo. Katika Data Na. 6(a) na 6(b), mofu {(-)i-} imejitokeza katika vivumishi vya pekee *ingine* {(i)-ingine} na *yote* {i-ote}. Katika vivumishi vyote hivyo, mofu hiyo imejitokeza mwanzoni kama kawaida pamoja na vivumishi vya pekee, ilhali vivumishi hivyo vimeshirikiana na nomino zilizokopwa kutoka lugha ya Kifaransa (*madivision, projet*). Kuhusu Data Na. 7(a-c), mofu {(-)i-} imejitokeza katika kuwezesha ushirikiano wa nomino na maneno mengine yanayoandamana nayo yakiwa na hadhi ya vivumishi vya a-unganifu. Katika Data Na. 7(a), mofu {(-)i-} imejitokeza katika *ya huyu* {i-a-/huyu}. Katika Data Na. 7(b), mofu {(-)i-} imejitokeza katika *ya kwanza* {i-a-/kwanza} ambapo katika Data Na. 7(c) mofu hiyohiyo imejitokeza katika *ya wapi* {i-a-/wapi}. Katika sentensi zote tatu, ujitokezaji wa mofu {(-)i-} umetokana na upatanisho wa kisarufi kutokana na nomino za Kifaransa *question* na *article* ambazo zilitumiwa katika Kiswahili zikiingizwa katika ngeli ya I-ZI. Aidha, katika Data Na. 7(b) matumizi ya mofu {(-)i-} yametokana na nomino ya Kiswahili *nyimbo* ya ngeli I-ZI.

Kutokana na ufafanuzi uliotolewa kulingana na Data Na. 1-7, imeonekana kuwa mofu {(-)i-} inatambulika katika Kiswahili cha nchini Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ikijitokeza katika mazingira tofauti. Hivyo, imejitokeza kama kiambishi kipatanishi cha ngeli baina ya nomino na kivumishi au nomino na kitenzi au kama kiambishi awali cha mtendwa au mtenda wa jambo. Hii ina maana kuwa, katika Kiswahili cha nchini Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, matumizi ya mofu {(-)i-} hayapingani na dhima ya kimofosintaksia ya ngeli yoyote au kiambishi ngeli chochote kinachotambulika katika Kibantu. Hata hivyo, kutokana na mifano iliyotolewa hapo juu, utambuzi na mazingira ya utokezaji wa mofu hiyo vimeweka bayana hali yake ya kutozingatia kanuni za upatanisho wa kisarufi kwa baadhi ya miktadha ya kimatumizi.

5.2 Asili ya Kisarufi na Uamilifu wa Mofu {(-)i-}

Kujitokeza kwa mofu {(-)i-} katika vitenzi na vivumishi ni ishara kwamba kuwapo kwa mofu hiyo kumetokana na maneno yaliyoandamana na vipashio hivyo vya kiisimu, hasa nomino, kwani ndizo zilizo na hadhi ya kutawala upatanisho wa kisarufi katika tungo au sentensi. Jambo hili linaelekeza kufafanuliwa kwa namna mofu {(-)i-} inavyojitokeza katika Kiswahili kinachozungumzwa katika nchi za Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Hivyo, katika sehemu hii kutaangaziwa namna ambavyo mofu {(-)i-} inajidhihirisha kisarufi na uamilifu wake katika Kiswahili kinachozungumzwa katika maeneo hayo.

5.2.1 Mofu {(-)i-} kama Kibadala cha Viambishi Ngeli vya Ngeli zingine Zozote

Muundo wa sentensi zilizokusanywa kutoka katika vipindi mbalimbali vya redio zinazosikika mjini Bujumbura, zikiwa Burundi au Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, umedhihirisha hali tofauti, na baadhi yake zikiwa kinyume cha kawaida kwenye Kiswahili sanifu. Data Na. 8 inaonesha namna nomino zinazotokana na ngeli mbalimbali zinavyunganishwa na maneno mengine katika sentensi, upatanisho ukifanyika kwa mofu {(-)i-}.

Data Na. 8

(a) Shida *inayoonekana* ni ile problème ya ulozi.

Mofu undaji: {i-na-yo-on-ek-an-a}

→ Shida inayoonekana ni ile ya ulozi/Ulozi ndiyo shida kuu.

(b) Wakitujulisha kuwa (h)iyoy shida *ipo*.

Mofu undaji: {i-po}

→ Wakitujulisha kuwa hiyo shida ipo.

(c) Walipata shida ya hiyi mtoni.

Mofu undaji: {i-a-}

→ Walipata shida kutokana na mto huu.

(d) Mambo moja ya *kazi imesemeka...*

Mofu undaji: {i-me-sem-ek-a}

→ Jambo moja la kikazi lililosemekana...

(e) *Akili yake iko* « qu'est-ce que... »

Mofu undaji: {i-ake-/i-ko}

→ Akili yake ikoje ?

(f) Kama mtu *iko* na kosa fulani, ...

Mofu undaji: {i-ko}

→ Kama mtu ana kosa fulani.

(g) Mambo hii *iko inapatikana* mbele ya umati ya watu wote.

Mofu undaji: {i-ko-/i-na-pat-ikan-a}

→ Mambo haya yalitokea hadharani.

(h) Kwa ajili ya maendeleo ya kijiji *yetu*.

Mofu undaji: {i-etu}

→ Kwa ajili ya maendeleo ya kijiji chetu.

Katika Data Na. 8(a-c), mofu {(-)i-} imejitokeza kulingana na nomino za ngeli ya I-ZI ya Kiswahili sanifu. Katika Data Na. 8(a), mofu {(-)i-} katika {i-na-yo-on-ek-an-a} imewakilisha uhusiano baina ya kitenzi *inayoonekana* na nomino *shida* iliyotumiwa katika umoja, na ambayo kwa kawaida ni ya ngeli ya I-ZI. Kwa upande mwingine, mofu {(-)i-} imejitokeza katika Data Na. 8(b) katika kitenzi kishirikishi *ipo* kulingana na nomino hiyohiyo *shida*. Pia, katika Data Na. 8(c), mofu {(-)i-} iliyojitokeza katika kiunganishi ya {i-a} imetokana na uwapo wa nomino *shida* ambayo ni ya ngeli ya I-ZI katika Kiswahili sanifu.

Vilevile, katika Data Na. 8(d-e), mofu {(-)i-} imejitokeza kulingana na nomino zilizoandamana na maneno yaliyohusisha mofu hiyo {(-)i-}. Katika Data Na. 8(d), ujitokezaji wa mofu {(-)i-} katika *imesemeka* {i-me-sem-ek-a} umechochewa na ukawaida wa nomino *kazi* ambayo ni ya ngeli ya I-ZI. Hali hii imejitokeza katika Data Na. 8(e) ambapo mofu {(-)i-} iliyo katika kivumishi kimilikishi *yake* {i-ake} imetokana na nomino *akili* ambayo kivumishi hicho kimeshirikishwa nayo, ilhali katika kitenzi kishirikishi *iko* {i-ko}, mofu {(-)i-} imetokana na uhusiano wa kisarufi baina ya kitenzi hicho na nomino ileile *akili* ambayo ni ya ngeli ya I-ZI.

Katika Data Na. 8(f-h), mofu {(-)i-} imejitokeza kulingana na nomino ambazo si za ngeli ya I-ZI. Katika Data Na. 8(f), mofu {(-)i-} imejitokeza katika kitenzi *iko* {i-ko} ikiwakilisha uhusiano baina ya kitenzi hicho na nomino *mtu* ya ngeli ya A-WA. Pia, imejitokeza katika Data Na. 8(g) ikiwakilisha uwiano baina ya kifungutenzi *iko inapatikana* {i-ko-/i-na-pat-ikan-a} na nomino *mambo* ya ngeli ya LI-YA, ilhali katika Data Na. 8(h) mofu hiyo imejitokeza katika kivumishi *yetu* {i-etu} ikisimamia uwiano baina ya kivumishi hicho na nomino *kijiji* ya ngeli ya KI-VI.

Kutokana na ufafanuzi kuhusiana na Data Na. 8(a)- (e), mofu {(-)i-} ambayo kwa kawaida yake ni kiambishi ngeli cha ngeli ya I-ZI (Habwe na Karanja, 2012; Matinde, 2018), imetumiwa kuunganisha vitenzi au vivumishi na nomino za ngeli hiyohiyo I-ZI (shida, kazi, akili). Pia, katika Data 8(f)- (h), mofu {(-)i-} imejitokeza ikiunganisha vitenzi au vivumishi na nomino (kwa umoja au kwa wingi) ambazo si za ngeli ya I-ZI (mtu, mambo, kijiji). Hivyo, ni bayana kuwa, katika Kiswahili cha Afrika ya Kati, ngeli hiyo {(-)i-} hutumika ikiwa na dhima ya kusimamia nomino bila kuzingatia ngeli ya nomino husika, bali kwa kuwakilisha ngeli zozote.

5.2.2 Mofu {(-)i-} kama Kiashiria cha Umoja na Wingi

Katika lugha za Kibantu, ngeli huaminika kama viashiria vya idadi, kwa sababu ngeli yoyote huwa na hadhi ya kudhihirisha umoja na wingi wa nomino husika. Kwa kawaida, hasa katika Kiswahili sanifu, ngeli yoyote inakusanya nomino ambazo kila moja hutumiwa katika umoja na wingi, kila hali miongoni mwa hizo mbili ikiwa na sifa na ishara yake ya kimuundo (Habwe na Karanja, 2012). Hivyo, nomino za ngeli moja huwa na sifa zinazofanana, hivi kwamba mwonekano wa kimuundo wa nomino, yaani mofu zinazounda neno husika, hasa zile zinazowakilisha umoja na wingi, hutoa angalau fununu ya ngeli ambapo nomino husika inapatikana. Kwa hiyo, sentensi zifuatazo hudhihirisha namna mofu {(-)i-} inavyotumika kwa kuashiria idadi katika Kiswahili cha nchini Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Data Na. 9

(a) Hii mzigo zaidi *ililemea* wamama na mabinti.

- Mofu undaji: {i-li-lem-e-a}
 → Huu mzigo uliwalemea mama na binti zao.
 (b) Hii jambo *inakuwa inasumbua* wakinamama.
 Mofu undaji: {i-na-ku-w-a}/ {i-na-sumbu-a}
 → Hili jambo linawasumbua akina mama.
 (c) Mama yake *iko* innocente.
 Mofu undaji: {i-ko}
 → Mama yake hana hatia.
 (d) Hiyo shamba *inapelekwa*.
 Mofu undaji: {i-na-pelek-w-a}
 → Hilo shamba linaporwa na wengine.
 (e) Kila jimbo *iko* na spécificité yake.
 Mofu undaji: {i-ko}
 → Jimbo lolote huwa na upekee wake.

Data Na. 10

- (a) Atanako nayo ni jina ya mtu.
 Mofu undaji: {i-a-/mtu}
 → Atanako nalo ni jina la mtu.
 (b) Nakamata pia *hiyo* neno ya nani?... Honorable Omeri alisema.
 Mofu undaji: {ha-i-o}/ {i-a}
 → Nikariri pia hotuba ya nani?... Mheshimiwa Omeri alisema.
 (c) Mko na *ile* uwezo ya kwenda kuwaona wakubwa wetu na kuwaambia.
 Mofu undaji: {i-le}/ {i-a/ kwenda}
 → Mna uwezo wa kwenda kuwaona wakuu wetu na kuongea nao.
 (d) Jina *yake* kabisa ni Didier Kalonji.
 Mofu undaji: {i-ake}
 → Jina lake la kweli ni Didier Kalonji.

Katika Data Na. 9(a-e), mofu {(-)i-} imejitokeza katika vitenzi vilivyohusika kwenye sentensi hizo zote ikiashiria umoja wa nomino zilizoandamana navyo. Nomino *mzigo* [9(a)], *jambo* [9(b)], *mama* [9(c)], *shamba* [9(d)] na *jimbo* [9(e)] ambazo zinatokana na ngeli za U-I (*mzigo*), A-WA (*mama*), na LI-YA (*jambo*, *shamba*, *jimbo*) zimetumiwa katika umoja. Wakati huohuo, ingawa nomino tajwa hapo juu zinatofautiana katika kuzingatia ngeli, zimetumiwa kwa umoja. Hali hii inawakilishwa na mofu {(-)i-} katika vitenzi *ililemea* {i-li-lem-e-a} [9(a)], *inakuwa inasumbua* {i-na-ku-w-a}/ {i-na-sumbu-a} [9(b)], *iko* {i-ko} [9(c)], *inapelekwa* {i-na-pelek-w-a} [9(d)] na *iko* {i-ko} [9(e)].

Kwa upande mwingine, katika Data Na. 10(a)- (d), mofu {(-)i-} imejitokeza katika vivumishi vilivyoshirikiana na baadhi ya nomino zilizohusika katika sentensi hizo, zikiwa katika hali ya umoja. Hivyo, vivumishi ya *mtu* {i-a-/mtu} [10(a)], *hiyo* {ha-i-o} [10(b)], *ile* {i-le} [10(c)] na *yake* {i-ake} [10(d)] vimetumika kueleza nomino *jina* [10(a), 10(d)], *neni* [10(b)] na *uwezo* [10(c)] zilizo katika umoja. Hali hii inawakilishwa na mofu {(-)i-}. Katika sehemu ifuatayo, data zilizowekwa

zinaonesha namna mofu {(-)i-} inavyoashiria dhana ya wingi nomino zikiwa katika hali ya wingi au za wingi.

Data Na. 11

(a) Mambo ya uchawi *inakuwa* kama fléo.

Mofu undaji: {i-na-ku-w-a}

→ Mambo hanayohusu uchawi yamekuwa kama janga/Uchawi umekuwa kama janga.

(b) Mambo hii *iko inapitikana* mbele ya umati ya watu wote.

Mofu undaji: {i-ko-/i-na-pit-ik-an-a}

→ Mambo haya yalitokea hadharani.

(c) Manyumba yake *ilijengwa* kwa samani kubwa.

Mofu undaji: {i-li-jeng-w-a}

→ Nyumba zake zilijengwa kwa gharama kubwa.

(d) Maredio yetu *inafanya* kazi nyingi.

Mofu undaji: {i-na-fany-a}

→ Redio zetu zinafanya kazi nyingi.

Data Na. 12

(a) Maisha ya mtu *ina* samani.

Mofu undaji: {i-na}

→ Maisha ya mtu yana thamani.

(b) Magumu *iko* kwako na kwa mwingine.

Mofu undaji: {i-ko}

→ Magumu yanajitokeza kwako na kwa wengine.

(c) Ile maafa yote *inafanyikana* « vue » ya watu yote.

Mofu undaji: {i-na-fany-ik-an-a}

→ Yale maafa yote yanafanyika/yanajitokeza hadharani.

(d) Ile mauwaji yote *iko inafanyika* mbele ya services za l'Etat zenye ziko impuissants zenye hazi-intervenir.

Mofu undaji: {i-ko-/i-na-fany-ik-a}

→ Mauwaji yote yale yanafanyika bila sekta mbalimbali za serikali kuweza kuyazuia.

(e) Aussi longtemps mujakazi *iko* na biake yote, na mauwaji *itaendelea* na solution haitakuwa.

Mofu undaji: {i-ta-end-el-e-a}

→ Iwapo mjakazi ana uwezo wake ule, mauwaji yataendelea kujitokeza bila suluhisho.

(f) Ulozi *inaweza* kusemea tangu zamani.

Mofu undaji: {i-na-wez-a}

→ Ulozi unajulikana tangu zamani.

(g) Uhimizaji *iwe* ya kweli katika jamaa.

Mofu undaji: {i-w-e}

→ Uhimizaji utekelezwe kiukweli katika jamii.

Katika Data Na. 11(a-d), nomino zimehusisha mofu {(-)i-} ikiashiria wingi. Katika Data Na. 11(a) na 11(b), nomino *mambo*, wingi wa *jambo* (ngeli ya LI-YA katika Kiswahili sanifu) imeandamana na vitenzi *inakuwa* {i-na-ku-w-a} [11(a)] na *iko inapitikana* {i-ko-/i-na-pit-ik-an-a} [11(b)] ambapo hali ya wingi imeashiriwa na mofu {(-)i-}. Pia, katika Data Na. 11(c) na 11(d), nomino *manyumba* [11(c)] na *maredio* [11(d)] zimeshirikiana na vitenzi *ilijengwa* [11(c)] na *inafanya* [11(d)] ambapo upatanisho wa kisarufi umedhihirishwa na mofu {(-)i-}.

Vilevile, katika Data Na. 12(a)- (g), mofu {(-)i-} imetumika katika vitenzi ikiwakilisha nomino za wingi. Kwa mujibu wa Matinde (2016), nomino za wingi ni zile zinazoashiria dhana ya wingi, hivi kwamba si rahisi kugawika na kuwa kitu kimojakimoja. Hivyo, nomino *maisha* [12(a)], *magumu* [12(b)], *maafa* [12(b)], *mauwaji* [12(d)/(e)], *ulozi* [12(f)] na *uhimizaji* [12(g)] ambazo ni za wingi zimeshirikiana na vitenzi *ina* {i-na} [12(a)], *iko* {i-ko} [12(b)], *inafanyikana* {i-na-fany-ik-an-a} [12(c)], *iko inafanyika* {i-ko-/i-na-fany-ik-an-a} [12(d)], *itaendelea* {i-ta-end-el-e-a} [12(e)], *inaweza* {i-na-wez-a} [12(f)] na *iwe* {i-w-e} [12(g)] ambapo upatanisho wa kisarufi umedhihirishwa na mofu {(-)i-} iliyotumika ikiashiria dhana ya wingi.

Kulingana na data Na. 9, 10, 11 na 12, mofu {(-)i-} imetumiwa ikiashiria umoja au wingi wa nomino. Hili lilifanyika katika muktadha wa kimfosintaksia, lakini, bila kuzingatia ngeli asili ya nomino. Uchambuzi wa data umeonesha kuwa nomino zilizomo katika umoja zimeshirikiana na vitenzi na upatanisho wa kisarufi ukiwakilishwa na mofu {(-)i-}. Kwa upande mwingine, mofu hiyohiyo imetumiwa kama kipatanishi cha ngeli baina ya nomino zilizomo katika wingi na vitenzi. Hivyo, ni dhahiri kuwa mofu {(-)i-} ina hadhi ya kuashiria upatanisho wa kisarufi katika umoja na wingi, hali ambayo si ya kawaida katika matumizi ya ngeli kwani, kila moja miongoni mwa hali ya umoja na wingi ina sifa na ishara yake ya kimuundo (Habwe na Karanja, 2012).

5.2.3 Mofu {(-)i-} kama Kiambishi cha Upatanisho wa Kisarufi

Kama ilivyohakikishwa na wanasarufi miundo, tungo/sentensi huundwa na mfuatano wa viambajengo ambavyo hupishana kihadhi, yaani kiambajengo kidogo hushirikiana na kiambajengo chenye hadhi sawa katika kuunda kiambajengo kikubwa (Bloomfield, 1963; Matinde, 2018). Hii ina maana kwamba, tungo/sentensi huundwa kwa maneno yanayoshirikiana, moja likihusiana na jingine, hali ambayo maneno katika tungo huwa na uhusiano wa karibu zaidi ya maneno mengine ambayo hayahusishwi katika muungano wa tungo. Katika lugha za Kibantu, uhusiano huo hudhihirishwa na upatanisho wa kisarufi ambapo umoja na wingi wa ngeli za nomino husika huathiri umbo zima la kisintaksia. Hivyo, katika matumizi ya mofu {(-)i-}, ni dhahiri kuwa mofu hiyo imehusika katika kushirikisha maneno, hasa nomino na maneno mengine katika tungo/sentensi.

Data Na. 13:

(a) Namna gani biashara *itatusaidia*.

Mofu undaji: {*i-ta-tu-saidi-a*}

→ Biashara itatusaidiaje ?

(b) Shida *inayoonekana* ni ile problème ya ulozi.

Mofu undaji: {*i-na-yo-on-ekan-a*}

→ Shida ya ulozi ndiyo inayotawala siku hizi.

(c) Walipata shida ya *hii* mtoni.

Mofu undaji: {*i-a-/hii*}

→ Walipata shida kutokana na mto huu.

(d) Akili *yake* iko “qu’est-ce que je vais faire aujourd’hui par rapport” ya wakubwa *yetu* ?

Mofu undaji: {*i-ake*}/ {*i-etu*}

→ Anafikiria: ninaweza kufanya nini siku hizi, kulingana na wakubwa wetu?

Katika Data Na. 13(a-d), mofu {(-)i-} imehusika katika kuoanisha nomino na maneno ya aina zingine, yaani vitenzi na vivumishi. Vitenzi *itatusaidia* {*i-ta-saidi-a*} [13(a)], *isikilize* {*i-siki-l-iz-e*} [13(b)] na *inayoonekana* {*i-na-yo-on-ekan-a*} [13(c)] vimepatanishwa na nomino *biashara* [13(a)] na *Shida* [13(b)] ambazo kiasili ni za ngeli ya I-ZI ya Kiswahili sanifu. Pia, vivumishi ya *hii* {*i-a-/hii*} [13(c)] na *yake* {*i-ake*} [13(d)] vimepatanishwa na nomino *shida* [13(c)] na *Akili* [13(d)] ambazo nazo ni za ngeli hiyo. Katika mifano hii, nomino za ngeli ya I-ZI zimeathiri vitenzi ambavyo vimeambikwa mofu {(-)i-} ambayo imetumika kama kipatanishi cha ngeli baina ya nomino na vitenzi. Kwa upande mwingine, nomino za ngeli hii ya I-ZI zimechochea upatanisho baina ya mashina ya vivumishi ambavyo yameambikwa na kuathiriwa na mofu {(-)i-}.

Kutokana na maelezo hayo, imedhihirika kuwa katika launi tofauti za Kiswahili cha Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, ngeli ya I-ZI hutumika kama ilivyo katika Kiswahili sanifu, kwa sababu nomino za ngeli hiyo huwa na uamilifu kama ule ilio nao katika Kiswahili sanifu. Data zifuatazo zinaonesha namna mofu {(-)i-} inavyowakilisha upatanisho wa kisarufi bila kuzingatia ngeli ya nomino husika.

Data Na. 14

(a) Hiyo shamba *inapelekwa*.

Mofu undaji: {*i-na-pelek-w-a*}

→ Hilo shamba linaporwa na wengine.

(b) Kama mtu *iko* na kosa fulani, ...

Mofu undaji: {*i-ko*}

→ Kama mtu ana kosa fulani.

(c) Maisha ya mtu *ina* samani.

Mofu undaji: {*i-na*}

→ Maisha ya mtu yana thamani.

(d) Mambo hii *iko inapatikana* mbele ya umati ya watu wote.

- Mofu undaji: {i-ko-/i-na-pat-ikan-a}
 → Mambo haya yalitokea hadharani.
 (e) Kwa ajili ya maendeleo ya kijiji yetu.
 Mofu undaji: {i-etu}
 → Kwa ajili ya maendeleo ya kijiji chetu.
 (f) Jina yake kabisa ni Didier Kalonji.
 Mofu undaji: {i-ake}
 → Jina lake la kweli ni Didier Kalonji.

Katika Data Na. 14(a- f), mofu {(-)i-} imejitokeza katika sentensi ikiwa na hadhi ya kipatanishi cha ngeli baina ya nomino za ngeli mbalimbali na maneno mengine bila kuzingatia ngeli ya nomino husika wala umoja na wingi. Vitenzi *inapelekwa* {i-na-pelek-w-a} [14(a)], *iko*{i-ko} [14(b)], *ina*{i-na} [14(c)] na *iko inapatikana* {i-ko-/i-na-pat-ikan-a} [14(d)] vimeunganishwa na nomino *shamba* (ngeli ya LI-YA) [14(a)], *mtu* (ngeli ya A-WA) [14(b)], *maisha* (ngeli ya YA-YA) [14(c)] na *mambo* (ngeli ya LI-YA) [14(d)] ambazo si za ngeli ya I-ZI. Ingawa nomino hizo si za ngeli ya I-ZI, kuunganishwa kwake kwa vitenzi na vivumishi husika kumewezeshwa na mofu {(-)i-}. Vilevile, nomino *kijiji* (ngeli ya KI-VI) [14(d)] na *jina* (ngeli ya LI-YA) [14(f)] zimepatana na vivumishi *yetu* {i-etu} [14(d)] na *yake* {i-ake} [14(d)] kwa mofu {(-)i-}.

Kutokana na maelezo hapo juu, tofauti na yanayotambulika katika Data Na. 13, Data Na. 14 inaonesha upatanisho wa kisarufi usioashiria uwiano baina ya nomino na vitenzi wala nomino na vivumishi, kwani upatanisho umedhihirishwa na mofu {(-)i-} ambapo nomino zenyewe si za ngeli ya I-ZI. Vilevile, data hizo zinaonesha matumizi ya mofu {(-)i-} pasi na kuzingatia umoja wala wingi.

Data Na. 15

- (a) Justice *itakuwa* ku deux niveau.
 Mofu undaji: {i-ta-ku-w-a}
 → Sheria itazingatiwa kwenye pande zote.
 (b) Formation *inamsaidia* kujikomporte mzuri.
 Mofu undaji: {i-na-m-saidi-a}
 → Elimu inamsaidia kujiheshimisha.
 (c) Fondation *ina* shabaha ya kuboresha maisha ya wakazi wa Kabare.
 Mofu undaji: {i-na}
 → Shirika lina shabaha ya kuboresha maisha ya wakazi wa Kabare.
 (d) Orchestre *iliitwa* Joli nom.
 Mofu undaji: {i-li-it-w-a}
 → Kwaya iliitwa “Joli nom”.
 (e) Kupima projet *yote itapita*.
 Mofu undaji: {i-ote-/i-ta-pit-a}
 → Kuchunguza mradi wote utakaopatikana.
 (f) Usikilize upate émission *yako*.
 Mofu undaji: {i-ako}

→ Usikilize/ufuatilie kama kipindi chako kimepitishwa (redioni).

Katika Data Na. 15(a-f), kumedhihirika jambo lingine ambalo si la kawaida katika Kiswahili sanifu, isipokuwa kwa Kiswahili cha Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, hasa baadhi ya jamiilugha za Kiswahili katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Jambo hilo ni sawa na ujitokezaji wa msimbo wa Kifaransa unaotokana na uzoefu wa lugha hiyo katika maisha ya raia wa nchi hizo, aghalabu Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Katika Data Na. 15(a)- (e), mofu {(-)i-} imejitokeza katika vitenzi *itakuwa* {i-ta-ku-w-a} [15(a)], *inamsaidia* {i-na-m-saidi-a} [15(b)], *ina* {i-na} [15(c)], *iliitwa* {i-li-it-w-a} [15(d)] na *itapita* {i-ta-pit-a} [15(e)] ambapo imewakilisha upatanisho wa kisarufi baina ya vitenzi hivyo na nomino *justice* [15(a)], *formation* [15(b)], *fondation* [15(c)], *orchestre* [15(d)] na *projet* [15(e)]. Vilevile, nomino *émission* [15(f)] imepatanishwa na kivumishi {i-ako} [15(e)] kwa msaada wa mofu {(-)i-} ikitumika kama kipatanishi cha ngeli baina ya nomino na vivumishi tajwa hapo juu.

Kutokana na maelezo hapo juu, katika Data Na. 15, mofu {(-)i-} imedhihirika kuashiria upatanisho wa kisarufi, kwani imejitokeza ikiwa na dhima ya kuunganisha nomino na vitenzi. Vilevile, Data Na. 15 imeonesha namna matumizi ya Kiswahili yanavyoathiriwa na lugha ya Kifaransa ambayo ndiyo lugha rasmi na ya kufundishia nchini Burundi na katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Mifano iliyotolewa hapo juu imedhihirisha matumizi ya msamiati wa Kifaransa katika Kiswahili, kwani, wanajamiilugha wa Kiswahili hasa wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo hujikita katika ukopaji sisisi, pale ambapo Kiswahili chenye kina msamiati wa kueleza dhana husika (Nassestein & Bose, 2020). Katika muktadha huo, nomino za Kifaransa huwakilisha nomino za Kiswahili. Hivyo, ni dhahiri kuwa ujitokezaji wa msimbo wa Kifaransa katika Kiswahili cha nchini Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo huchochea upatanisho wa kisarufi unaowakilishwa na mofu {(-)i-} inayojitokeza kama kipatanishi cha ngeli baina ya nomino na maneno mengine yanayoiandamia katika tungo, yaani vitenzi na vivumishi.

6.0 Hitimisho

Makala hii imeshughulikia uamilifu wa mofu {(-)i-} katika Kiswahili cha nchini Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ambacho baadhi ya wanazuoni, bila kutofautisha launi zake, walikiita Kingwana. Utafiti huu umetambulisha mazingira ya ujitokezaji wa mofu {(-)i-} kutoka katika sentensi mbalimbali zilizokusanywa kutoka katika vipindi mbalimbali vya Kiswahili vinavyorushwa na redio za Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ambazo husikika mjini Bujumbura. Matokeo ya utafiti huu yamedhihirisha uamilifu wa mofu {(-)i-} kwa namna tofauti. Kwanza, mofu {(-)i-} hujitokeza kama kibadala cha viambishi ngeli vya ngeli zingine zozote zile kwa sababu inahusisha nomino ambazo zinapatikana katika ngeli zingine ambazo si ngeli ya I-ZI. Kwa mantiki hii, mofu {(-)i-}

imedhihirisha uwezo wa kuwakilisha upatanisho wa kisarufi baina ya nomino ambazo kwa asili yake ni za ngeli ya I-ZI au ngeli zingine zozote na maneno mengine yanayozindamia katika tungo. Pili, mofu {-i-} imedokeza hali ya uwili, kwani imetambulika kama ishara ya “idadi-pacha” kwa maana kwamba, inadokeza ama dhana ya umoja au ya wingi. Ujitokezaji wa mofu {-i-} umedokeza kutopatana kwa viambishi vinavyounda tungo, ama sivyo, mofu hiyo inadhihirisha maana/mofimu ambazo ziko katika ngeli zingine, hali ambayo inaipa uamilifu wa kuziwakilisha. Kwa upande mwingine, matokeo ya utafiti huu yanaamsha wazo la kufikiria tena mfumo wa ngeli kwa kuzingatia si tu Kiswahili sanifu, bali lahaja zingine za Kiswahili. Hivyo, kama alivyosema Renée Maran (1921/1969) na kusisitizwa na Butoyi (2009), wanaisimu wanapaswa kufanya tafiti zaidi.

Marejeleo

- Ally, N.H. (2020) *Athari za Mofu Ambishi na Nyambulishi katika Uundaji wa Vitenzi vya Kisambaa*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dar es Salaam.
- Bakari, K.B. (2015) *Ulinganishi wa Kiisimu kati ya Lahaja ya Kipemba na Kitumbatu*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Bloomfield, L. (1963) *Language*. New York: Holt.
- Butoyi, D. (2009) *Etude Lexicographique du Dictionnaire Français-Kirundi de Van Der Burgt: Contribution à la Confection Scientifique d'un Dictionnaire Bilingue*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Burundi, Bujumbura.
- _____ (2022) *Tathmini ya Makosa ya Kisarufi ya Wanafunzi wa Kingwana Wanaojifunza Kiswahili Sanifu: Uchunguzi Kifani wa Vyuo Vikuu vya Burundi*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dar es Salaam.
- Chomsky, N. (1981) *Lectures on Government and Binding: The Pisa Lectures*. Dordrecht : Foris.
- Ferrari, A., Kalunga, M. na Mulumbwa, G. (2014) *Le Swahili de Lubumbashi. Grammaire, Textes, Lexique*. Paris: Karthala.
- Fradin, B. (2003) *Nouvelles Approches en Morphologie*. Paris: Presses Universitaires de France.
- Goyvaerts, D. (2007) “Bukavu Swahili: Tense, Aspect and Blurry History”. *Journal of Asian and African Studies*, Juz. Na. 74: 5-33.
- Habwe, J. na Karanja, P. (2012) *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Hassan, H.S. (2016) *Ujidhihirishaji wa Mofu Zinazowakilisha Nafsi na Njeo katika Kiswahili: Utafiti Linganishi wa Lahaja ya Kipemba na Kiswahili Sanifu*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Maran, R. (1921/1969) *Batouala, Véritable Roman Nègre*. Paris: Albin Michel.

- Masebo, J.A. na Nyambari, C.M. (2016) *Nadharia ya Lugha, Kiswahili 1: Kidato cha 5 na 6*. Dar es Salaam: Nyambari Nyangwine Publishers.
- Matinde, R.S. (2018) *Dafina ya Lugha, Isimu na Nadharia. Kwa Sekondari, Vyu vya Kati na Vyu Vikuu* (Toleo la pili). Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) Ltd.
- Mutaka, N.M. (2000) *An Introduction to African Linguistics*. München: LINCOM Europa.
- Mwashota, P. (2017) “Ujitokezaji wa Viambishi Njeo na Athari zake Kifonolojia katika Lugha ya Kibantu: Mifano kutoka Lugha ya Shimalila”. *Kioo cha Lugha*, Juz. Na. 14(1): 25-38.
- Nassenstein, N. na Bose, P.B. (2020) “Morphological Features of Kiswahili Youth Language(s): Evidence from Dar es Salaam, Goma, Lubumbashi and Nairobi”. *Linguistics Vanguard*, Juz. Na. 6(4): 1-13.
- Nshimirimana, E., Tuyubahe, P. na Misago, J.M. (2020) Le Morphème -ag- dans le Kingwana. *ODISSEIA*, Juz. Na. 5(1): 1-21.
- Nurse, D. na Hinnebusch, T.J. (1993) *Swahili and Sabaki: A Linguistic History*. California: University of California Press.
- Onyango, J.O. (2012) *Historical Development of Kiswahili*. Nairobi: Kenyatta University Press.
- Polome, E.C. (1967) *Swahili Language Handbook*. Washington: Center for Applied Linguistics.